

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



**S. L.P 1575,  
Iringa.  
Simu: (026) 2700157  
Nukushi: (026) 2703014  
Barua pepe:  
[rbciringa@pccb.go.tz](mailto:rbciringa@pccb.go.tz)  
Mtandao : [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)**

---

---

**IRINGA 25 JUNI, 2020**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI  
VIONGOZI WA KIJJI CHA IDODOMA MKOANI DODOMA  
WAKAMATWA KWA RUSHWA MKOANI IRINGA**

**Ndugu Wanahabari,**

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Iringa inatarajia kuwafikisha Mahakamani Kaimu Mtendaji wa Kijiji YAHAYA MALIMO CHAMLE na Mwenyekiti wa Kijiji cha Idodoma Kata ya Malola Wilaya ya Mpwapwa Mkoa wa Dodoma kwa kosa la kushawishi, kuomba na kupokea rushwa ya Shilingi. **1,000,000/=** kinyume na kifungu cha 15 (1) (a) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007.

Uchunguzi wa TAKUKURU Mkoa wa Iringa ulibaini kuwa, mnamo tarehe 23/06/2020 watuhumiwa wakiwa katika eneo la Gangilonga (Hospitali ya IMECC) katika Manispaa ya Iringa, waliomba na kupokea rushwa ya shilingi 1,000,000/= kutoka kwa Daktari OMARI SHABANI LUSHINO anayemiliki ardhi ekari 66 zilizopo Kijiji cha Idodoma ili aweze kusaini na kuweka mhuri wa Kijiji katika Hati ya Kimila ya kumiliki eneo hilo.

**Ndugu Wanahabari**

Mlalamikaji Daktari OMARI SHABANI LUSHINO baada kuombwa rushwa ya Shilingi milioni moja na watuhumiwa, akaamua kutoa taarifa katika Ofisi ya TAKUKURU Mkoani Iringa, ambapo baada ya wachunguzi kujiridisha na uwepo wa mazungira ya rushwa mtego wa rushwa uliandaliwa na watuhumiwa

walikamatwa baada ya kupokea fedha za mtego wakiwa tayari wamesaini na kuweka mhuri katika hati hizo.

**Ndugu Wanahabari,**

Uchunguzi wa tuhuma hii umekamilika na TAKUKURU Mkoa wa Iringa inatarajia kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani leo Juni 25, 2020 katika Mahakama ya Wilaya ya Iringa. Kesi hii itaendeshwa na Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa inatoa wito kwa wakazi wote wa mkoa wa Iringa kutofumbia macho Rushwa na wanaojihusisha na vitendo vya Rushwa na kwamba inaendelea kuwasihi kutoa taarifa sahihi kwa TAKUKURU ili hatua stahiki zichukuliwe.

***Penda nchi yako, kataa rushwa.***

***Imetolewa na :-***

***SGN***

***Mweli Evert Kilimali,***

***MKUU WA TAKUKURU MKOA WA IRINGA***